

MAIGIZO KATIKA NYIMBO ZA ARUSI ZA JAMII YA WAIMENTI


NA

STELLA MIRIKO JULIUS

BEDA/112/03856

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA IDARA YA ELIMU ILI
KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA ELIMU
KATIKA CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

OKTOBA 2015



IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza maigizo katika nyimbo za arusi za jamii ya Waimenti. Utafiti ulilenga kuonyesha maingiliano baina ya maigizo na nyimbo za arusi. Pia ulilenga kuchunguza umuhimu wa maigizo katika nyimbo za arusi katika jamii ya Waimenti huku ukibainisha baadhi ya nyimbo za arusi katika jamii hiyo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mguso ambapo mguso unaotolewa na kazi ya fasihi kwa hadhira yake husisitizwa . Kila kazi ya fasihi hulenga kwa njia moja au nyingine mtu/watu fulani hata kama hadhira hiyo ni nafsi ya mtunzi husika. Kazi ya fasihi hutoa mguso wa aina fulani kwa hadhira ili ifikirie na kujiuliza maswali au hata kutoa funzo fulani. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo na kitakwimu. Baada ya kuchanganua data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa njia ya majedwali. Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ilishughulikia utangulizi wa tasnifu. Hapa mtafiti alifafanua mada ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo wa utafiti. Sura ya pili imeangazia historia fupi ya jamii ya Waimenti ambao ndio watafitiwa, mapitio ya maandishi yanayohusu utanzu wa maigizo na nyimbo, tafiti zilizofanywa awali na watafiti wengine pamoja na misingi ya nadharia. Mtafiti amefafanua Mifumo ya kisiasa ya Waimenti, utamaduni wao pamoja na imani zao. Sura ya tatu imeshughulikia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika kukusanya data , kuichanganua na kuiwasilisha. Utafiti huu ulinuiwa kuwasaidia wanafunzi kutambua maingiliano baina ya maigizo na nyimbo za arusi za Waimenti. Pia ulikusudiwa kuonyesha dhima ya maigizo katika nyimbo za arusi. Kupitia kwa utafiti huu jamii ya Waimenti inahimizwa kushikilia na kuhifadhi utamaduni wake.